

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS

SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Kumb. Na. JA.9/259/A/97

08 Juni, 2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Katibu wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Maji anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi **mbili (2)** kama zilivyoainishwa katika tangazo hili.

1.0 WIZARA YA MAJI

Wizara ya Maji ilianzishwa ikiwa ni utekelezaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 36 ambayo inampa Mheshimiwa Rais wa Nchi mamlaka ya kuanzisha Ofisi mbalimbali zikiwemo Wizara. Majukumu ya Wizara ni kutayarisha na kusimamia utekelezaji wa Sera, Mikakati na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, kutayarisha na Kusimamia sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia Sekta ya maji, kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji, kukusanya, kuchambua, kutafsiri na kuhifadhi takwimu muhimu za Sekta ya maji, kutoa miongozo ya kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za maji, kutoa miongozo ya utoaji wa huduma za maji na kuratibu majukumu na kutekeleza ushauri wa bodi ya taifa ya maji. Wizara ya Maji inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia mipango na maazimio ya maendeleo ya ndani na nje ya nchi kama vile Dira ya Taifa ya Maendeleo (TDV 2025); Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs 2016 – 2030); Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano; Kwa mujibu wa miongozo hiyo, malengo ni kuhakikisha kwamba wananchi waishio vijijini wanaopata huduma za maji safi inafikia zaidi ya **asilimia 85** na mijini zaidi ya **asilimia 95** ifikapo mwaka 2025.

1.0. Fundi Sanifu Msaidizi Maji II- NAFASI 2

1.0.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa wenye Elimu ya Sekondari na waliofuzu Mafunzo ya cheti cha ufundi kwa mwaka mmoja katika fani ya ujenzi (Civil) kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na wenye ujuzi wa kutumia kompyuta.

1.0.2 MAJUKUMU YA KAZI

- i. Uchukuaji wa sampuli za maji na udongo kwa ajili ya upimaji;
- ii. Kufanya matengenezo ya vifaa vya maabara ya kawaida na ya dharura yanapohitajika;
- iii. Kufanya upimaji wa maji na udongo wa maeneo ya miradi na kuandaa maelekezo ya matibabu yanayohitajika;
- iv. Kukusanyaji wa takwimu za hali ya maji na udongo zinazohitajika kwenye maeneo ya miradi;
- v. Kufanya uchunguzi wa sampuli za maji safi na majitaka kwa kutumia vifaa maalum (specialized equipment) kama vile *Atomic Absorption Spectrophotometer, Kjeldah* na mashine nyinginezo;
- vi. Kubaini viwango vya kiasi cha madawa yanayohitajika kwa kutibu na kusafisha maji (dosage);
- vii. Kufanya uchunguzi wa madawa ya kutibu na kusafisha maji; na
- viii. Kufanya kazi zingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi.

1.0.3 NGAZI YA MSHAHARA

Kwa kuzingatia ngazi ya mishahara ya Serikali. **TGS A/1**

MASHARITI YA JUMLA.

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45.
- ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
- iii. **Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingilia katika kada tofauti na walizonazo, wapitishie barua zao za**

maombi ya nafasi za kazi kwa Waajiri wao na Waajiri wajiridhishe ipasavyo.

- iv. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (**Detailed C.V**) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (**referees**) watatu wa kuaminika.
- v. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
 - Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificates.
 - Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI
 - Computer Certificate
 - Vyeti vya kitaaluma (Professional certificates from respective boards)
- vi. **Testimonials”, “Provisional Results”, “Statement of results”, hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**
- vii. **Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).**
- viii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- ix. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **21, Juni 2022.**
Muhimu, kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu. anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa;

**KATIBU
OFISI YA RAIS
SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA
S.L.P. 2320 DODOMA.**

- i. **Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo;**
<http://portal.ajira.go.tz/>
(Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa ‘Recruitment Portal’)

- ii. **Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.**

Limetolewa na;

**KATIBU
SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA**